

CHUO CHA UONGOZI WA MAHAKAMA LUSHOTO



TAARIFA KWA UMMA

MAHAKIMU MAHAKAMA ZA MWANZO NA WAJUMBE WA MABARAZA YA KATA WAKUMBUSHWA KUSIMAMIA HAKI

Januari 28, 2019 Mwanza,

Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto (IJA), kimewakutanisha Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo na Wajumbe wa Mabaraza ya Kata jijini Mwanza katika semina yenye lengo la kuwajengea uwezo katika majukumu yao ya usimamizi wa haki.

Akifungua mafunzo hayo ya siku tatu katika Ukumbi wa Mkuu wa Mkoa Mwanza, Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu Kanda ya Mwanza, Mheshimiwa Sam Mpayu Rumanyika amesema kuwa Mafunzo hayo ni utekelezaji wa agizo la **Mheshimiwa Jaji Mkuu Profesa Ibrahimu Hamis Juma**, baada ya ziara yake katika Mahakama Kuu Kanda ya Tabora mapema mwaka jana.

Katika ziara hiyo, Mheshimiwa Jaji Mkuu alipokea malalamiko kuhusu utendaji usioridhisha wa Mabaraza ya Kata, ambapo alishuhudia kuwa maamuzi mengi ya Mabaraza hayo hayakuthibitishwa na Mahakama za Mwanzo kama inavyoagizwa katika sheria iliyoanzisha Mabaraza hayo yaani *The Ward Tribunal Act, 1985*.

Ni kutokana na hilo Mheshimiwa Jaji Mkuu akaagiza kuendeshwa mafunzo yenye kuwajengea uwezo Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo pamoja na Wajumbe wa Mabaraza ya Kata juu ya majukumu ya Mabaraza ya Kata na usimamizi wa Mabaraza ya Kata unaofanywa na Mahakama za Mwanzo.

Kaimu Mkuu wa Chuo, Taaluma, Tafiti na Ushauri wa IJA, Ndugu Fahamu Mtulya amewaambia wanahabari kuwa mafunzo hayo yamelenga kuwawezesha washiriki, Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo na Wajumbe wa Mabaraza ya Kata kubadilishana uzoefu katika changamoto za utoaji haki sambamba na kuzitatua.

“Pamoja na Mambo mengine tutawakumbusha Muundo na Mamlaka ya Mahakama za Mwanzo vile vile Muundo na Mamlaka ya Mabaraza ya Kata, Ukomo wa mamlaka wa Mahakama za Mwanzo, Mashauri Katika Mahakama za Mwanzo, namna ya kusuluhisha mashauri katika Mabaraza ya Kata pamoja na Mamlaka ya Usimamizi ya Mahakama za Mwanzo kwa Mabaraza ya Kata” Alisisitiza Ndugu Mtulya.

Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo na Wajumbe wa Mabaraza ya Kata katika Mahakama Kuu Kanda ya Mwanza wanakuwa wanufaika wa pili wa mafunzo ya namna hiyo, baada ya wenzao wa Kanda ya Tabora kupatiwa mafunzo kama hayo mwaka jana.

Imetolewa na Kitengo cha Uhusiano.

Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto,

S.L.P. 20 Lushoto

Simu: 255-27-2660133

Barua pepe: info@ija.ac.tz, pro@ija.ac.tz

Tovuti: www.ija.ac.tz